# JARIDA LA MTANDAONI

## WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

*Toleo la 1, Januari, 2021*

**DKT. NDUGULILE AZIPA SIKU 30 TAASISI ZA UMMA ZINAZODAIWA NA TTCL KULIPA MADENI**



# DKT. NDUGULILE AHIMIZA TAASISI ZA SERIKALI KUTUMIA KITUO CHA TAIFA CHA DATA KUHIFADHI TAARIFA ZAO

**Na Prisca Ulomi, WMTH**

Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dkt. Faustine Ndugulile amehimiza taasisi za Serikali kutumia Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data (NIDC) kuhifadhi taarifa zao kwa kuwa ni sehemu salama, ina miundombinu na mifumo ya TEHAMA ya kisasa na ina wataalamu wabobezi na ina nafasi ya kutosha kwa ajili ya kupangisha mifumo.

Dkt. Ndugulile ameyasema hayo wakati wa ziara yake ya kutembelea NIDC, Dar es Salaam ambapo aliambatana na Naibu Waziri wake, Mhandisi Kundo A. Mathew, Katibu Mkuu, Dkt. Zainabu Chaula, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Waziri Kindamba na watendaji wa Wizara hiyo na kubaini kuwa ni taasisi 84 tu za Serikali zinatumia NIDC kati ya taasisi 149 zinazohifadhi taarifa zake kwenye kituo hicho.

Amezikumbusha taasisi za Serikali kuzingatia agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alilolitoa alipotembelea NIDC kuzindua Mfumo wa Kielektroniki wa Kukusanya Mapato (electronic Revenue Collection System - eRCS) mwaka 2017 ambapo umeiwezesha NIDC kuongeza makusanyo ya mapato yake kutoka shilingi bilioni 1.4 mwaka 2019 na kufikia shilingi bilioni 2.76 mwaka 2020.

Naye Naibu Waziri, Mhandisi Kundo A. Mathew ameipongeza NIDC kwa kutengeneza mifumo mbali mbali ya TEHAMA ambayo inaiwezesha Serikali kuongeza makusanyo ya mapato na kurahisisha maisha kuendana na mahitaji ya wananchi ikiwemo kulipa tiketi ya mabasi ya njia ya mtandao; kuweka mafuta kwenye gari; kulipa kiingilio kwenye uwanja wa mpira

wa Benjamin Mkapa; usafiri wa kivuko cha Kigamboni; usajili wa leseni BRELA; na maegesho ya magari uwanja wa ndege wa Dar es Salaam.

Katibu Mkuu, Dkt. Zainab Chaula amewaeleza watendaji wa NIDC washirikiane kwa karibu na wataalamu wa Wizarani ili kuhakikisha kuwa Serikali inaendelea kuwahudumia wananchi kwa kutumia TEHAMA ili kuokoa muda wao kutafuta huduma za Serikali badala yake watumie kufanya kazi na kuongeza uzalishaji mali.

Meneja wa NIDC, Geofrey Mpangala amesema kuwa wateja wanaotumia kituo hicho wamepunguza gharama za uendeshaji na uwekezaji kwenye taasisi zao kwa kuwa hawajengi miundombinu na mifumo ya TEHAMA; wateja wanapata viwango vya juu vya data yenye kasi na uhakika wa usalama wa data zao na huduma zinatolewa kituni hapo kwa saa 24.

Mkurugenzi Mkuu wa TTCL, Waziri Kindamba amemshukuru Dkt. Ndugulile kwa ziara yake kwa kuwa imeongeza ari na shauku ya utendaji kazi kwa wataalamu wa NIDC ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya wateja na mifumo ya TEHAMA ili kurahisisha huduma kwa wananchi.



*Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dkt. Faustine Ndugulile akisisitiza jambo kwa wafanyakazi wa Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data (hawapo pichani) wakati wa ziara yake ya kutembelea taasisi hiyo, Dar es Salaam. Anayesikiliza ni Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dkt. Zainab Chaula.*



Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dkt. Faustine Ndugulile akijadiliana jambo na Meneja wa Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data, Godfrey Mpangala (wa pili kushoto) wakati wa ziara yake kituoni hapo, Dar es Salaam. Wa kwanza kushoto ni Naibu Waziri, Mhandisi Kundo A. Mathew na wa tatu kushoto ni Katibu Mkuu, Dkt. Zainab Chaula, wote wa Wizara hiyo.



Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Kundo A. Mathew akizungumza na wafanyakazi wa Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data (hawapo pichani) wakati wa ziara ya Waziri wa Wizara hiyo, Dkt. Faustine Ndugulile (hayupo pichani) ya kutembelea taasisi hiyo, Dar es Salaam. Kushoto ni Meneja wa taasisi hiyo, Geofrey Mpangala.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dkt. Zainab Chaula akizungumza na wafanyakazi wa Kituo cha Kuhifadhi Data (hawapo pichani) wakati wa ziara ya Waziri wa Wizara hiyo, Dkt.Faustine Ndugulile (wa kwanza kushoto) ya kutembelea taasisi hiyo. Wa nne kulia nia Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Mawasiliano Tanzania, Waziri Kindamba.



Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dkt. Faustine Ndugulile akijadiliana jambo na Meneja wa Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data, Godfrey Mpangala (wa pili kushoto) wakati wa ziara yake kituoni hapo, Dar es Salaam. Wa kwanza kushoto ni Naibu Waziri, Mhandisi Kundo A. Mathew na wa tatu kushoto ni Katibu Mkuu, Dkt. Zainab Chaula, wote wa Wizara hiyo.

# DKT. NDUGULILE AIPA TCRA MIEZI MITATU KUMALIZA CHANGAMOTO ZA VIFURUSHI NA BANDO KWA WANANCHI

**Na Prisca Ulomi, WMTH**

Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dkt.Faustine Ndugulile amei-pa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) miezi mitatu kumaliza changamoto za ban-do na vifurushi zinazotolewa na kampuni za simu za mkononi kwa wananchi.

Dkt. Ndugulile ameyasema hayo wakati wa ziara yake alipotembelea TCRA ikiwa ni moja ya taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo kwa lengo la kufa-hamiana, kutambua majukumu yao na kuzungum-za na Bodi, Menejimenti na wafanyakazi wa taasisi hiyo ili kuwa na uelewa wa pamoja na kushirikiana kwa kufanya kazi kwa pamoja katika kuhudumia wananchi kuelekea Mapinduzi ya Nne ya Viwanda na kuiwezesha Tanzania kuwa na uchumi wa kidiji-tali.

Ameongeza kuwa TCRA ishughulikie malala-miko ya wananchi kwa kuwa wananchi hawana imani na vifurushi na bando, na kuwe na mfumo wa kuhakiki gharama halisi za mawasiliano kuendana na fedha aliyotoa mwananchi na kuwe na namba ya bure ambayo wananchi watapiga ili kuwasilisha malalamiko yao ili kuwawezesha wananchi kuonge-za imani yao kwa Serikali.

Amesisitiza kuwa ni heri tufanye maamuzi ma-baya kuliko kutokufanya maamuzi na amewataka washirikiane na Baraza la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA – CCC) kumaliza changamoto hiyo kwa kuwa watanzania sio wajinga, anataka aone kapata shilingi moja anaitumia shilingi moja yake kupiga simu.

Pia, amehimiza wahakikishe kuwa chaneli tano za bure za runinga zinaonekana hata baada ya muda wa kulipia kumalizika kwa kuwa chaneli hizo hazionekani kwenye baadhi ya ving'amuzi.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Mhandisi Kundo A. Mathew ameipongeza TCRA kwa kutengeneza mifumo ya TEHAMA, kutambua changamoto zilizopo na imejipanga kuzifanyia kazi kwa kuwa lazima TEHAMA ichukue nafasi yake na itufikishe watanzania tunakotaka kwenda.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dkt.Zainab Chaula amewataka wafanyakazi wa TCRA kujiongeza na kujituma zaidi badala ya kusubiri maagizo na maelekezo kwa kuwa wao ni wataalamu, hivyo washirikiane kwa pamoja ili kuhakikisha kuwa wanaendelea kuwahudumia watoa huduma na watumiaji wa huduma za mawasiliano.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Mhandisi James Kilaba amekiri uwepo wa changamoto za bando na vifurushi na ameahidi kuzifanyia kazi kwa kuwa TEHAMA imeongeza mnyororo wa thamani kwenye sekta zote na imesogeza huduma mbali mbali viganjani.




*Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dkt. Faustine Ndugulile akisisitiza jambo kwa Menejimenti ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (hawapo pichani), wakati alipotembelea taasisi hiyo, Dar es Salaam.*



*Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Kundo A. Mathew (wa tatu kushoto) akiuliza utendaji kazi wa mitambo ya kufuatilia matumizi ya masafa kwa Jumanne Ikuja (wa kwanza kushoto), Mhandisi wa masafa wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, wakati wa ziara ya kutembelea taasisi hiyo, Dar es Salaam. Anayesikiliza wa pili kushoto ni Waziri wa Wizara hiyo, Dkt. Faustine Ndugulile.*



*Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dkt. Faustine Ndugulile (wa pili kushoto) na Naibu Waziri wake, Mhandisi Kundo A. Mathew (wa tatu kushoto) wakimsikiliza Mhandisi Jumanne Ikuja akiwaeleza kuhusu gari lenye mitambo maalumu linalofuatilia matumizi ya masafa wakati wa ziara yao Mamlaka ya mawasiliano Tanzania, Dar es Salaam. Wa nne kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Mhandisi James Kilaba.*



*Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dkt. Faustine Ndugulile (katikati) akipata maelezo kuhusu makumbusho ya mawasiliano kutoka kwa Raphael Mwango, Afisa Makumbusho wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania wakati wa ziara yake kwenye taasisi hiyo, Dar es Salaam. Wa kwanza kulia ni Naibu Waziri wa Wizara hiyo,*



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dkt. Zainab Chaula akizungumza na wafanyakazi wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (hawapo pichani) kabla ya kumkaribisha Waziri wa Wizara hiyo, Dkt. Faustine Ndugulile (anayesikiliza) kuzungumza wakati wa ziara yake ya kutembelea taasisi hiyo, Dar es Salaam.*

# DKT. NDUGULILE AZIPA SIKU 30 TAASISI ZA UMMA ZINAZODAIWA NA TTCL KULIPA MADENI

**Na Prisca Ulomi, WMTH**

Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dkt. Faustine Ndugulile amezipa siku 30 taasisi za umma zinazodaiwa na Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) kulipa madeni kwa Shirika hilo ili liweze kujiendesha, kutekeleza majukumu yake ya kutoa huduma ya mawasiliano ya sauti na data kwa taasisi za Serikali, sekta binafsi na wananchi ili kukuza uchumi na kuchangia pato la taifa.

Dkt. Ndugulile ameyasema hayo wakati wa ziara yake alipotembelea TTCL kwa lengo la kufahamiana na kuzungumza na wajumbe wa Bodi, Menejimenti na wafanyakazi wa TTCL, Dar es Salaam ambapo aliambatana na Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Mhandisi Kundo A. Mathew na Mejimenti ya Wizara hiyo.

Ameongeza kuwa zaidi ya taasisi 20 za Serikali zinadaiwa na TTCL zaidi ya kiasi cha shilingi bilioni 30 ambapo zipo taasisi zinatumia huduma za mawasiliano za TTCL na zinakusanya mapato ya zaidi ya shilingi bilioni moja kwa mwezi ila hawako tayari kulipa huduma za TTCL.

Vile vile, ametoa onyo kali kwa kampuni zinazohujumu miundombinu ya TTCL ili ishindwe kutoa huduma za mawasiliano kwa wateja wake kuwa waache tabia hiyo mara moja na wafanye biashara kwa misingi ya ushindani, vinginevyo Serikali itawachukulia hatua kali.

Aidha, amesisitiza kuwa kwa watakaoiba nyaya za shaba za TTCL na kuuza kama chuma chakavu nao waache mara moja kwa kuwa watahusishwa na uhujumu uchumi kwa kudhoofisha utendaji kazi wa TTCL na kwa watakaobainika watachukuliwa hatua kali na Serikali kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama.

Amewataka watendaji wa Wizara kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kufanya utafiti na tathmini ya kubaini mchango wa Sekta hii aidha wa moja kwa moja au usio wa moja kwa moja katika kukuza uchumi na kuchangia pato la taifa kwa kuwa taasisi za Serikali, sekta binafsi na wanachi wanatumia huduma za mawasiliano ya data na sauti na kuendesha shughuli mbali mbali za kiuchumi na kijamii kwa kutumia TEHAMA.

Naye Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Mhandisi Kundo A. Mathew amewataka watumishi wa TTCL kuwa wabunifu na kuacha kufanya kazi kwa mazoea na wajenge utaratibu wa kufuata na kuwahudumia wateja huko waliko badala ya kusubiri wateja kuwafuata ofisini.

Mkurugenzi Mkuu wa TTCL, Waziri Kindamba amesema kuwa amepokea maelekezo ya Waziri, Dkt. Ndugulile na ametoa rai kwa watumishi wote wa TTCL kujituma ili kuongeza upatikanaji wa huduma ya mawasiliano yenye kasi ya brodibandi kutoka asilimia 49 mwaka 2020 hadi kufikia asilimia 80 mwaka 2025.



*Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Mawasiliano Tanzania, Waziri Kindamba akifafanua jambo kwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dkt. Faustine Ndugulile (wa kwanza kulia) kuhusu mitambo ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano wakati wa ziara yake kwenye Shirika hilo, Dar es Salaam. Wa pili kulia ni Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Mhandisi Kundo A. Mathew*



*Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dkt. Faustine Ndugulile akisisitiza jambo wakati akikagua miundombinu ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano wakati wa ziara yake kwenye Shirika la Mawasiliano Tanzania, Dar es Salaam. Kulia ni Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Mhandisi Kundo A. Mathew na kushoto ni Mhandisi wa Shirika hilo, Marick Urassa.*




*Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Kundo A. Mathew akisisitiza jambo kwa wafanyakazi wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (hawapo pichani) wakati wa ziara ya Waziri wa Wizara hiyo, Dkt. Faustine Ndugulile (anayesikiliza) alipotembelea Shirika hilo, Dar es Salaam.*



*Mhandisi wa Mtandao wa Shirika la Mawasiliano Tanzania, Amina Daudi akitoa maoni yake kwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dkt.Faustine Ndugulile (hayupo pichani) wakati wa kikao na wafanyakazi alipotembelea Shirika hilo, Dar es Salaam.*




*Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dkt. Faustine Ndugulile akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Mawasiliano Tanzania, Waziri Kindamba kuhusu mtambo wa zamani wa kupiga simu kwenye chumba cha makumbusho cha Shirika hilo wakati wa ziara yake ya kutembelea Shirika hilo, Dar es Salaam*

**Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
**Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**
**S.L.P. 677,40470 Dodoma, Tanzania**
**Barua pepe: ps@mawasiliano.go.tz**
**Tovuti: www.mawasiliano.go.tz**
**Instagram: @WizaraMTH**
**Twitter: @WizaraMTH**